

Musa Alelewa Katika Nchi ya Misri

KUTOKA SURA YA 1-2

Chagua mazoezi yanayofaa mahitaji na mapendezi ya mtoto wako.

Fanyeni mazoezi hayo mkiwa familia.



SOMA KUTOKA SURA YA 1-2

Kisha, someni Hadithi ya Biblia Iliyochorwa (kwenye Intaneti au kwenye karatasi iliyochapishwa), na mzungumzie maswali mwishoni mwa somo.

MAZOEZI ZAIDI UNAYOWEZA KUCHAPISHA



MAZOEZI YA PICHA

UKURASA WA KUPAKA RANGI Someni tena Kutoka 2:1-10. Waombe watoto wadogo (miaka 3 hadi 5) wakisie majina ya watu watatu walio kwenye picha. Mwishowe, waombe wapake rangi picha.



MAZOEZI YA KUJIFUNZA

NASABA Waombe watoto wakubwa (miaka 6 hadi 10) wajaze majina ya watu wa ukoo wa Musa. Soma maandiko kwa madokezo zaidi.



KUSANYA NA UJIFUNZE

KADI YA MHUSIKA WA BIBLIA Soma mambo machache kumhusu.

Uliza maswali yaliyo kwenye kadi. Tumia kadi zote ulizo nazo kucheza mchezo ufuatao: Mtu mmoja wa familia achague kadi bila wengine kuona amechagua kadi ipi. Kisha awaulize wale wengine katika familia maswali ili kumtambulisha mhusika aliye kwenye kadi iliyochaguliwa. Anapaswa kuuliza maswali yatakayojibiwa kwa kusema ndio au la. Kwa mfano, Je, mhusika ni mwanamume? Je, aliishi kabla ya Yesu? Je, alimtumikia Yehova? Mzazi au mtoto mkubwa anaweza kuwasaidia watoto wadogo ikihitajika.

Mazoezi yanayopatikana katika ukurasa huu yanapatikana kwenye tovuti ya jw.org/sw.

(Tazama kwenye MAFUNDISHO YA BIBLIA > WATOTO > MIRADI YA IBADA YA FAMILIA.)